**HALMASHAURI YA WILAYA YA KALIUA**
S.L. P 83,KALIUA, **Simu Na:**+255262965679,+255262965676,+255622225618
**Barua pepe:** ded@kaliuadc.go.tz,
**Tovuti:** www.kaliuadc.go.tz
Barabara ya Ulinduanoni/ Ufukutwa

Kumb. Na. KDC/M.2/VOLII/0056/104 06/02/2020

# TANGAZO LA KAZI YA KUJITOLEA

Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua inawatangazia Wananchi wote nafasi za kazi ya Watendaji wa Vijiji wa kujitolea kwa wote wenye sifa kama ifuatavyo;-

## A. WATENDAJI WA VIJIJI (NAFASI 29)

### 1. Sifaza Mwombaji

Awe na Elimu ya Kidato cha nne (Form Four) au Sita (Form Six) aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti (NTA LEVEL 5) katika moja ya fani Zifuatazo;- Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo Dodoma au chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

### 2. Kazi za kufanya

i. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya kijiji
ii. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa amani na msimamizi wa Utawala Bora katika kijiji
iii. Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya kijiji
iv. Katibu wa mikutano na kamati zote za Halmashauri ya kijiji
v. Kutafsiri na kusimamia Sera,sheria na Taratibu
vi. Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali
vii. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya kitaalamu katika Kijiji



Scanned by CamScanner

viii.Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za kijiji
ix. Mwenyekiti wa kikao cha wataalamu waliopo katika kijiji
x. Kupokea, kusikiliza na kutatua migogoro ya wananchi
xi.Kusimamia utungaji wa sheria ndogo za kijiji
xii. Kusimamia ukusanyaji wa mapato katika kijiji
xiii. Kuandaa na kutunza rejista ya Wakazi wote wa kijiji
xiv. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata

**3. MASHARTI YA JUMLA**

1. Mwombaji awe raia wa Tanzania
2. Mwombaji awe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45 na awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai au kufungwa jela.
3. Maombi yote yaambatanishwe na maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed cv).
4. Maombi yote yaambatanishwe na nakala za vyeti vya taaluma, vyeti vya elimu (IV au VI

**4.** Maombi yatumwe kwa:-

MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA,
S.L.P.83,
**KALIUA.**

Tarehe ya mwisho ya kupokea maombi ni tarehe 19/02/2020 saa 9.30 mchana.

Dkt. John M. Pima
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**HALMASHAURI YA WILAYA**
**KALIUA**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA KALIUA
S.L.P. 83
KALIUA

*Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)*

Scanned by CamScanner